

ASb  
approved



Kiswahili

# Barua kwa Mama

Ursula Nafula  
Catherine Groenewald



Mama alizweka  
nguo zake katika  
begi ndogo.



Alinikumbatia  
akasema, "Kwa  
heri kwa sasa."

"Mama unaenda  
wapi?" Nilimuuliza.






Nilianza kulia  
nikitaka kumfuata.

Baba alinibeba  
akanituliza.



Baba alisema,  
"Mamako anaenda  
hospitalini  
kujifungua mtoto."



Niliposikia 'mtoto'  
sikulia tena.

"Kwa nini aende  
hospitalini?"



Baba alinijibu,  
"Nitakueleza kwa  
nini anaenda  
hospitalini."

Baba alinieleza lakini sikuelewa.

Nilimuuliza, "Ataendelea kunipenda?"



Alinieleza,  
"Tutakupenda  
wakati wote."



"Ninaweza  
kumwandikia  
barua akiwa  
huko?" Nilimuuliza  
baba.



Jioni hiyo, nilianza  
kumtungia mama  
baru.



Nilichukuwa  
karatasi na kuanza  
kuandika.



Mama, mama!  
Baba alisema  
kwamba umeenda  
kumleta mtoto  
mwingine.



Tafadhali, fanya  
haraka urudi  
nyumbani.



Ningependa  
umlete mtoto  
msichana.

Nitacheza naye  
akiwa mkubwa.



Unaweza kuwaleta  
wawili.

Mmoja atakuwa  
wangu.



Ninakusubiri hapa  
nyumbani.



Niliikunja barua  
yangu ili baba  
ampelekee mama.

Asubuhi, barua  
haikuwepo.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Barua kwa Mama

Author - Ursula Nafula

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Catherine Groenewald

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

